

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, anapenda kuutarifu Umma kuwa kwa mwezi Januari 2024, Manispaa imepokea kiasi cha **Tshs.1,364,200,000.00** kutoka serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **04** ya vyumba vya madarasa, ujenzi wa vyumba **49** vya madarasa pamoja na ujenzi wa matundu ya vyoo **104**.

Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika Jedwali hapa chini:

NA	JINA MRADI	KIASI POKELEWA
1.	Ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa	50,000,000
2.	Ujenzi wa vyumba vya madarasa 49	1,127,000,000
3.	Ujenzi wa Matundu ya vyoo	187,200,000
JUMLA		1,364,200,000

Tunamshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha hizo ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za sekondari.

Maono yako katika sekta ya elimu ni dira kwetu, tunakuahidi kusimamia miradi kikamilifu na kuhakikisha inakamilika kwa wakati uliopangwa ili yaweze kutumika.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO

MANISPAA YA SINGIDA,

25 JANUARI,2024